*IOSR Journal Of Humanities And Social Science (IOSR-JHSS)*
*Volume 23, Issue 9, Ver. 7 (September. 2018) 39-46*
*e-ISSN: 2279-0837, p-ISSN: 2279-0845.*
*www.iosrjournals.org*

# Itikadi katika Riwaya za *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) za S. A. Mohamed

Jesseemurithii
*Murithi Joseph Jesse, Richard Makhanu Wafula na Geofrey Kitula King'ei*
*Wote wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.*
*Corresponding Author: Jesseemurithii*

**Ikisiri**
Makala hii inanuia kuonesha kuwa itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu kulingana na maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia. Itikadi ndiyo huelekeza misimamo, mielekeo na imani ya mtunzi na hivyo kuathiri mtazamo wa mwandishi kuhusu ulimwengu unaomzunguka, ambao huweza kubadilika kulingana na wakati na mahitaji ya kijamii. Katika mkabala huo makala hii inalenga kutathmini itikadi ya mtunzi katika riwaya za *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) za S. A. Mohamed. Kwa kutumia riwaya hizo, makala hii inatarajia kuthibitisha kwamba, itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu na hutangamana na jinsi mtunzi anavyobadilisha mikakati yake ili kukidhi mahitaji ya jamii lengwa kiwakati.

Date of Submission:16-09-2018 Date of acceptance: 01-10-2018

## I. UTANGULIZI

Itikadi ni dhana changamani na imeleta mijadala mingi miongoni mwa wanazuoni. Dhana hii ni telezi kwa sababu inaweza kufasiriwa kwa namna tofautitofauti kutegemea madhumuni na dhamira ya mtumiaji. Kwa hivyo, itikadi ni jumla ya mfumo wa mawazo, fikra na imani, inayoongoza na kumwelekeza mtunzi katika kuwasilisha ulimwengu wake kwa masuala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Itikadi ndiyo humuongoza mtunzi kuteua namna atakavyotekeleza majukumu yake ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kulingana na Chuachua (2011), itikadi ndiyo dira ituelekezayo kwenye sababu za mtunzi kupendekeza au kukemea jambo fulani. Kwa hiyo, itikadi hutuonesha namna mtunzi alivyotekeleza mafunzo yake, dhamira na falsafa yake na hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa uandishi wake. Itikadi ni maoni na mwenendo wa kufikiri juu ya maisha ya mwanadamu na jamii yake katika vipengele vya siasa, uchumi, dini, utamaduni na masuala ya kijamii kwa ujumla (Adorno na wenzake, 1950). Hii ina maana kuwa, itikadi waliyonayo wanajamii kuhusu maisha, ndiyo itakayowaongoza katika kufikiri na kutafakuri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao, kwa maana ya kufanikiwa au kutokufanikiwa. Mawazo haya yanapatikana pia katika Loewestein (1953) ambaye anaeleza kwamba, itikadi ni imani na tafakuri inayoeleza mtazamo wa mwanadamu kuhusu mfumo mzima wa maisha ya mwanadamu. Kwa mantiki hiyo, itikadi ni mfumo wa imani ambao unaeleza, unajumuisha na kufafanua masuala ya madaraka, haki za binadamu na kutathmini masuala ya kihistoria na maendeleo yake ili kufanya maamuzi sahihi kwa wakati uliopo na ujao.

Jessee (2017) anaeleza kuwa wahakiki wengi husema kwamba mtunzi hutawaliwa na itikadi moja ambayo hufumbata msimamo wake, kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utunzi wake. Akiwanukuu Mbatiah (1990) na Njogu (1997) anaeleza kwamba Mohamed ametawaliwa na itikadi ya Ujamaa katika baadhi ya kazi zake kama katika *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980) na *Kiza katika Nuru* (1988). Jessee anaonesha kuwa itikadi zinazojitokeza katika riwaya za awali za S. A. Mohamed ambazo ni *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* ni umwinyi na ubepari. Katika makala hii tumeangazia riwaya za *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) za S. A. Mohamed, kwa madhumuni ya kuonesha itikadi yake jinsi ilivyo badilifu na nyumbufu.

## II. ITIKADI KATIKA *DUNIA YAO*

Katika sehemu hii tunazungumzia itikadi iliyotawala katika riwaya hii, hususan itikadi ya utandawazi na itikadi ya kimapinduzi katika kuyatazama mambo ya ulimwengu.

### 2.1 Itikadi ya Utandawazi

Utandawazi ni mchakato wa kuunganisha uchumi, siasa, jamii, uhusiano wa tamaduni na kadhalika baina ya nchi. Utandawazi unaifanya dunia kuwa kijiji kimoja kisichokuwa na mpaka. Utandawazi unasisitiza uondoaji wa vikwazo vya kibiashara na kuifanya dunia kuwa soko moja, unahimiza soko huria, demokrasia,

utawala bora, usawa wa kijinsia na haki za binadamu (Thomas, 2005). Aidha, utandawazi ni mtazamo ambao huiangalia dunia kama moja na tangamano. Mtunzi anayeamini katika utandawazi huzungumzia mambo yanayoiathiri dunia nzima. Huweza kuchora wahusika wanaoweza kukubalika katika ulimwengu na mandhari ya kazi yake.

Said Ahmed Mohamed amejadili masuala mbalimbali ambayo yanadhihirisha itikadi tawala katika riwaya ya *Dunia Yao*, kuwa ni ya utandawazi. Baadhi ya masuala hayo ni ndoa, mapenzi, magonjwa, elimu, uchumi, sheria, siasa, uongozi, dini na mengineyo yanayoonesha kuridhia itikadi ya kitandawazi. Wahusika wake wamepewa sifa za kimataifa na mawazo yaliyopevuka. Mandhari ya dunia nzima imesawiriwa kwa majina ya "Peponi" na Motoni". Mtindo wa kinjozi umetumiwa kumwezesha kuwasafirisha wahusika wake kwa kadiri apendavyo. Haya yote yanadhihirisha jinsi mwandishi anavyoongozwa na itikadi ya utandawazi katika kuyatazama mambo ya ulimwengu mzima.

Kuhusu mfumo wa kiuchumi, kupitia kwa Bi. Mize, Mohamed anaonesha kuwa dunia anayoichunguza inazingatia mfumo wa ubepari. Aidha anaonesha kuwa, dhana ya utandawazi inatumiwa kuhalalisha mfumo huu kandamizi kote duniani. Mataifa yenye nguvu na mamlaka yanapendekeza sera na mifumo isiyo rafiki kwa uchumi wa mataifa machanga ambayo hulenga kuzinufaisha nchi zilizoendelea. Hivyo mataifa hayo yanaendelea kunawiri, huku mataifa machanga yakizidi kuwa masikini. Uhusiano huo unadhihirisha kuwa utandawazi ni asasi ya kiitikadi inayotumiwa na mataifa yenye nguvu kuendeleza mifumo ya ubepari inayoyanufaisha.

Mtunzi anaonesha namna utandawazi unavyoimarika kimataifa kutokana na teknolojia mpya, kama vile kompyuta, kampuni za mtandao, barua pepe na vyombo vya habari. Mwandishi anamsawiri Ndi, anayeisifu talakilishi aliyoletewa na Mtima binti yake (uk. 6). Pia, maneno ya Mtima kwenye barua aliyomtumia babake akimwambia kuwa atakapokwishakujifunza kuitumia barua pepe kuzungumza, wangewasiliana vizuri.

Itikadi ya utandawazi inazidi kujitokeza pale ambapo Ndi anasimulia jinsi alivyojifunza kompyuta kwa bidii, kwani alijua ni mwokozi wake katika maisha ya upweke na unyamavu kiasi cha kuihuisha (uk.11). Aidha, mwandishi anasimulia kuhusu kampuni ya mtandao ambayo inawezesha mazungumzo kupitia barua pepe ambayo Ndi anafurahia sana, ili wazungumze na bintiye Mtima. Pia, anaonesha kuwa kuna uhuru wenye hatari kutokana na usasa na mabadiliko ya haraka na hivyo Ndi anakerwa na bintiye Yungi aliyemkashifu na kumkemea hadharani.

Mwandishi anasema kuwa ubinafsi katika karne hii umeimarishwa na sayansi na teknolojia, na dunia imekuwa moja kwa sababu ya usahili wa uwazi wake na wepesi wa mawasiliano. Kwa mfano, maafa yakitokea pahala pamoja huenea duniani kote kwa sababu ya teknolojia (uk.48 – 49). Mwandishi anaonesha kuwa teknolojia inachangia kuenea kwa taarifa za maafa kwa kasi mno ulimwenguni, pamoja na kutohifadhiwa kwa utamaduni na maadili mabaya katika jamii kama vile ngono, ulevi, uchi, matusi, kelele, mavazi mabaya na madawa ya kulevya. Pia, kuna CD ya "*I need to know*" ya Marc Anthony na chombo cha kuendesha CD alichokinunua zamani katika safari alizopata kwenda London kikazi, alipokuwa mkuu wa idara ya matumizi (uk. 56).

Kuhusu elimu ambayo ni njia inayotumiwa kimakusudi na jamii kupitisha maarifa, ujuzi na maadili, kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine, mwandishi anaisawiri kama ambayo haithaminiwi sana siku hizi. Elimu inapuuzwa na waalimu wake wamepungukiwa maarifa kwa kuwa watoto wanafeli na mitihani inauzwa (uk. 42). Jambo hili linaonesha kuwa, elimu katika enzi ya utandawazi sio tiketi ya kupata kazi nzuri, bali ni asasi tu ya kuuendeleza ubepari wa kilimwengu. Mwandishi anaonekana kuamini kuwa elimu ni kipengele kimojawapo cha utawala ambapo walio na elimu ya juu hawafaidiki sana, huku wanaomiliki mifumo ya kiuchumi na biashara wakiendelea kutajirika na kujilimbikizia mali. Hili linafungamana na mkabala wa Althusser (1981) kuhusu itikadi kuwa, elimu ni asasi mojawapo inayotumiwa na watawala kuendeleza itikadi ya kitawala, ili kuhifadhi utabaka wao.

Mwandishi katika riwaya ya *Dunia Yao* anaona kuwa, utandawazi umekwishaondoa mipaka na kufanya ulimwengu jiji moja na kuathiri utamaduni. Mwandishi anaonesha imani yake kuwa, mavazi na mienendo ya Yungi imechangiwa kwa kiasi kikubwa na utandawazi (uk. 128). Kupitia mavazi ya Yungi, na jinsi anavyojibizana na baba yake kunaonesha imani ya mtunzi ya kuwa utandawazi umeleta ubinafsi kiasi cha kuwa hakuna anayemjali mwingine. Mtunzi anaonesha kuwa mabadiliko ya kitamaduni yamesababishwa na utandawazi na kufanya watu kuujali ubinafsi kuliko umoja na ushirikiano katika jamii zao. Pia, anaonesha jinsi wananchi wa kawaida wanavyoingia katika sherehe wakiwa wamevaa nusu uchi. Hali hii inaonesha namna utandawazi ulivyoathiri utamaduni wa dunia nzima na kuwa ni itikadi tu ya watawala wa nchi matajiri kuendeleza njama zao za kuendelea kutawala uchumi wa ulimwengu. Mwandishi anasema:

> Wengine wamevaa kama Mao, Lenin na wengine kama Gandhi. Kuna pia waliovaa ki-churchill au kirais wa US, wengine ki-cowboy au ki-Western (uk. 175).

Mwandishi anaamini kuwa utandawazi umeenea na umeathiri mavazi ya jamii yake ambayo imeuacha utamaduni wao na kuukumbatia wa kigeni. Majina yaliyomo kwenye dondoo iliyodokezwa ni ya viongozi waliowahi kuwa viongozi wa nchi za ng'ambo wala sio wa Kiafrika. Hali hiyo, inaonesha namna utandawazi ulivyoathiri dunia nzima, hasa Afrika.

Mohamed anaonesha msimamo wake kuwa kuna hatari zinazotokana na mambo ya kiteknolojia na utandawazi ambazo wengi wanakimbilia. Ogun mhusika ambaye ana sifa za kiungu, anaendelea kueleza wenyeji kuhusu athari za utandawazi, huku akionesha kuwa manufaa yake ni kwa nchi zenye mizizi ya utandawazi (uk. 192). Kwa hiyo, utandawazi ni jambo la hatari, na lenye athari mbaya kwa wenyeji kutegemea tu ubunifu wa nchi za kigeni hasa zile nchi zilizoendelea kwa sababu manufaa huwa ni kwao pekee (uk.193).

Kuhusu ndoa mwandishi anatuonesha utengano kati ya mume na mke mara kwa mara katika *Dunia Yao*. Kutokana na maelezo ya Sakarati, ndoa haiheshimiwi katika jamii kwa kuwa mkewe hakujali ndoa yao, mpaka anapoanza majuto walipopatwa na ugonjwa wa UKIMWI. Hii inaonesha ndoa zinavyokabiliwa na talaka, kuachana, pamoja na kunyimana haki za unyumba. Kwa jumla, mwandishi anaonesha jinsi mume anavyoyakimbia majukumu yake katika ndoa. Mhusika ambaye amewakilisha suala hili ni Ndi ambaye anayakimbia majukumu yake. Ndoa na familia inatumiwa tu kama asasi ya kuhalalisha maovu, na hivyo ni kigeu cha itikadi tawala ya kitandawazi.

Kuhusu dini ambayo ni imani maalum ya kuamini na kumtii Mungu wa haki, mtunzi ametaja dini za Kiislamu, Kikristo na Kibudha. Anasema dini ya Kiislamu ilitiliwa maanani alipokuwa mchanga, lakini siku hizi inatumiwa kuwadanganya watu na kuafikiana na mawazo ya Marx kuwa, dini ni ung'amuzi potoshi unaotumiwa na watawala kuendeleza itikadi tawala ya kitandawazi na kuuendeleza ubepari (Althusser, 1981). Hii ndiyo sababu inayowafanya watu wengi kuhama kutoka dini moja hadi nyingine jambo linalohusishwa na itikadi tawala ya kitandawazi. Ili kuendelea kudhibiti mataifa machanga na kimaskini dini inatumiwa kuwafanya watu wa nchi hizo kuendelea kuziamini huku mataifa ya Ulaya yakizidi kupiga hatua kimaendeleo (uk 141). Dini inatumiwa kama kipengele cha utawala wa kilimwengu wa kitandawazi, ili mataifa tajiri yaendelee kuhifadhi na kuendeleza utajiri, biashara na mifumo ya kiuchumi na utawala, huku mataifa yanayoendelea na ya kimaskini yakizidi kupotelea kwa dini mbalimbali, kwani hawana suluhu.

Siasa ni njia ya kufanya maamuzi katika taifa, mji au hata dunia nzima. Sehemu muhimu ya siasa ni majadiliano kati ya watu mbalimbali wenye nguvu au mamlaka. Katika demokrasia, kila mtu ana kiasi fulani cha nguvu. Kwa hivyo, siasa ya demokrasia ina maana ya watu wote huchangia maamuzi. Wakati mwingine haya hayawezekani kutokana na mambo kama vile utawala mbaya wa ukoloni mamboleo unaoleta jaribio la mapinduzi na maandamano ili kupigania haki. Mtunzi anaonesha kuwa siasa za kidemokrasia ni vigeu tu vya itikadi tawala ya kitandawazi, ambapo mataifa yenye nguvu hupendekeza mifumo yao ya kitawala kwa manufaa yao wenyewe.

Mtunzi anazungumzia sheria ambazo ni kanuni zinazoongoza nchi au jamii. Anatujulisha kuwa nchi haizingatii haki na sheria. Hata polisi wanapojua kuwa sheria haizingatiwi, hakuna anayeshughulika kuona haki inatendeka. Hivyo sheria ni asasi tu mojawapo ya kuendeleza itikadi ya watawala ya utandawazi, kama ambavyo Althusser (1981) anaeleza kuwa sheria hutumiwa kuendeleza itikadi ya kitawala, wala si kulinda haki. Aidha, mifumo ya kitawala kama demokrasia ni asasi mojawapo ya kunyamazisha watu, wala sio kwa masilahi yao.

Kuhusu utawala, ambayo ni shughuli nzima ya uongozi inayojumuisha mchakato wa kutoa uamuzi, kupitia kwa vikundi kama vile vyama vya kisiasa, mtunzi anasema kwamba, utawala ni jambo la kimsingi ambalo linapaswa kuzingatiwa kwa makini katika dunia nzima, la sivyo, dunia nzima inaweza kuangamia kutokana na utawala mbaya na wenye ukorofi na matumizi ya kimabavu. Polisi wanaiwakilisha serikali ya nchi na wanatumiwa kuwanyamazisha watu na kudhihirisha zaidi itikadi ambapo tabaka tawala huweza kutumia nguvu kama kuendeleza itikadi yao hata huko Ulaya.

**2. 2 Itikadi ya Kimapinduzi**

Mwandishi wa riwaya ya *Dunia Yao* anaendeleza itikadi ya mapinduzi ya marekebisho ya utandawazi. Kulingana na mwandishi, jamii yake imo katika kasi ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mabadiliko haya yanatokana na itikadi tawala ya utandawazi ambao umesababisha kasi kubwa ya kuwekeza kiuchumi na mabadiliko makubwa ya utamaduni. Mabadiliko haya, kwa sehemu kubwa, yanatokana na upeo wa matatizo ya kiuchumi yaliyosababishwa na masilahi ya kibiashara na utashi wa mataifa makubwa yanayolenga kila siku kupata faida kubwa kupita kiasi, kutokana na dhamira ya utandawazi kuwatawala binadamu. Mabadiliko mengi yanatokea kwa upande wa lugha, uchumi, mavazi, maadili, mila, utamaduni, dini, muziki, chakula na mengineyo (uk 41). Mwandishi anaonesha jinsi jamii ilivyoathirika na kubadilika kutokana na itikadi tawala ya utandawazi.

Mohamed katika riwaya ya *Dunia Yao* anasawiri mabadiliko makubwa ya matumizi ya lugha za kigeni. Mara kwa mara panatokea mchanganyo ndimi katika muundo na mtiririko wa riwaya. Jambo hili anaonekana kulifanya tu kimakusudi. Hii inaonesha kuwa amekumbatia mabadiliko kupitia uvunjaji wa kanuni za lugha.

Vilevile, tunaona utohozi wa hali ya juu hata kwa maneno yenye maana halisi kwa lugha ya Kiswahili. Haya yote yanatokana na athari za itikadi tawala ya utandawazi na kuonesha kuwa kwa upande mmoja anakubaliana na itikadi hii ya utandawazi na upande mwingine anaipinga. Anaona ni bora utandawazi ufanyiwe marekebisho au mabadiliko kadhaa ingawa uko sawa.

Aidha, mwandishi kupitia kwa Ndi anaonesha jinsi jamii yake ilivyopoteza hisia na jinsi mabadiliko yalivyosababisha maadili mabaya. Kutoathirika kwa Ndi na habari anazozipokea kutoka kwa Kilua kuwa Yungi anaugua UKIMWI kunaonesha mwandishi anaamini kuwa usasa unaoletwa na utandawazi umewafanya watu wa jamii yake kupuuza nguvu za kiasili, kwa vile wamebadilika kimawazo.

Mohamed anaamini kuwa dunia iko katika harakati za mabadiliko katika kila nyanja. Mabadiliko haya hayafai kwa nchi changa, kwani utandawazi ni itikadi inayoendelezwa na mataifa yaliyoendelea. Mataifa hayo hufanya hivyo ili yaendelee kuhifadhi nguvu zao za kiuchumi, kibiashara, kiutawala na kiteknolojia. Mataifa maskini na machanga huzidi kutumbukia kwenye lindi la umaskini kutokana na uongozi mbaya kwani asasi za utandawazi haziafikiani na malengo yao ya kitaifa na mazingira yao halisi. Hivyo, mtunzi anaupinga utandawazi kuwa haufai kwa mataifa machanga kutokana na kuleta madhara makubwa yaliyojidhihirisha.

Kwenye riwaya hii tumeshuhudia ubinafsi wa hali ya juu unaosababishwa na utandawazi ambapo hakuna mtu anayemjali mwenzake. Mtunzi anaonesha kuwa mapinduzi ya marekebisho ya utandawazi yanahitajika katika jamii ili kuondoa hali ya ubinafsi na kuwa na jamii yenye umoja na ushirikiano. Jamii ambayo inaweza kushiriki pamoja kwenye sherehe na hivyo kuonesha kuwa msimamo wake kuhusu mapinduzi sio mmoja. Aidha, anaonesha kuwa mabadiliko hutokana na maamuzi ya mtu binafsi wala sio matumizi ya nguvu kama katika *Kiza Katika Nuru* na *Asali Chungu* hivyo itikadi yake kuhusu mabadiliko ya kijamii imebadilika.

Kwa hivyo, itikadi ya mwandishi ni kwamba utandawazi umekuja kumomonyoa kila kitu katika jamii yake, kama vile utamaduni, shule, vyuo, desturi, mila, na heshima. Itikadi ya mwandishi kuhusu utandawazi ni kwamba una maafa mengi kuliko faida. Msimamo wake kuhusu utandawazi ni kwamba haufai na unapaswa ufanyiwe marekebisho kwa mataifa machanga, kwani ni itikadi inayoendelezwa na mataifa yaliyoendelea kujinufaisha na kuendeleza dhuluma na tawala zao katika mifumo ya kiuchumi, kibiashara na kiteknolojia.

## III. ITIKADI KATIKA *MHANGA NAFSI YANGU*

### 3.1 Itikadi ya Utandawazi

Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu,* itikadi tawala inayojitokeza ni ya utandawazi, hasa ukichunguza baadhi ya masuala kama vile mfumo wa kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia, mfumo wa elimu, utamaduni, asasi za utawala na mifumo ya sheria kati ya mingineyo. Mfumo wa kibepari unajitokeza katika riwaya hii. Mfumo huu una matabaka mawili ambayo ni tabaka la chini la watu wanaoishi kwa kufanya kazi na tabaka la juu la watu wanaoishi kwa kufanyiwa kazi. Mfumo huu unadhihirisha kuwa watu wachache wanajilikimbizia mali yote na kuwaacha maelfu na mamia ya watu wakiwa hawana chochote. Wanaoishi kwa kufanya kazi ndio wavuja jasho na msingi mkuu wa mfumo wa kibepari ni unyonyaji wa tabaka. Unyonyaji hautokani na nia mbaya ya mtu binafsi bali ni msingi wa mfumo wenyewe bila kujali nia au dhamira za watu waliomo katika mfumo huo. Mfumo huu wa kipebari pia huwa na sifa ya ulimbikizaji na uwekezaji wa mtaji ambao hutokana na ziada ili kuendeleza uzazi wa mfumo wenyewe**.**

Mwandishi anawaonesha Neshboch na Bw. Bawa wanavyoendeleza mfumo wa kipebari, pale wanapolijilimbikizia mali nyingi (uk. 140). Aidha, mali ilithaminiwa sana katika mfumo huu kiasi cha kwamba mali ndiyo huamua tabaka lao na maisha wanayoishi. Neshboch anaionea mali yake fahari kuu na anaitumia kumshawishi Afida akubali mapenzi yake. Naye, Afida kwa sababu ni zao la mfumo huu, anaamini kuwa akiolewa na tajiri, mali pia itakuwa yake. Hii inadhihirisha namna mfumo wa kibepari unavyoathiri watu kiasi cha kuuasi utu wao na kukubali kufanya lolote mradi wapate mali. Afida anaasi dini yake ya Kiislamu, anasahau watu wao kule motoni, anamtupa mpenzi wake Shaaban na mwishowe hata masomo anayaacha alipopachikwa mimba na Neshboch. Anadhihirisha kuwa mfumo huu wa kiuchumi huhalalishwa kwa kutumia itikadi inayotawala ya utandawazi ambapo waliopo katika mataifa machanga wanataka kusafiri kwenda kuishi mataifa ya ng'ambo ili kujinasibisha na utajiri na umaarufu wa mataifa hayo.

Mohamed anaonesha kuwa mfumo huu wa ubepari umesambaa kote ulimwenguni kupitia utandawazi na kusababisha umasikini mkubwa, kwani kadiri matajiri wanavyoendelea kuhodhi mali ndivyo masikini wanavyoongezeka. Hali hii, kama mtunzi anavyoonesha, husababishwa na mifumo ya kiuchumi ya kilimwengu hasa umwinyi, ubepari na utandawazi ambapo matajiri, humiliki nyenzo za uzalishaji mali na masikini hubakia hohehahe. Hali hizi huendelea kudumishwa kwa matumizi ya itikadi potofu ambazo huendelezwa na dini, utamaduni na asasi za serikali kama vile sheria, polisi, mahakama au ukubalifu na ukawaida tu. Mtunzi anadhihirisha kuwa hali hizi zinakuwa katika mataifa yote na hili linafanya kuamini kuwa itikadi inayojitokeza katika *Mhanga Nafsi Yangu* ni ya utandawazi kutokana na vile anavyowasilisha mfumo wa kiuchumi.

Mtunzi anaonesha namna pesa inavyochukuliwa kuwa ndiyo kila kitu huko Peponi. Pia, huonesha namna mfumo wa kiuchumi ulivyoathiri mataifa yote ulimwenguni. Kila kitu ni pesa, na maisha yao yote

hutegemea pesa. Mfumo wa kiuchumi uliopo katika jamii zetu ni wa kibepari ambao unapendelea mataifa ya Ulaya huku mataifa machanga ya Kiafrika yakizidi kuwa masikini. Nao Waafrika wanazikimbia nchi zao kama Afida, wakidhania maisha yatakuwa bora. Aidha, wanazidi kuumia kwani mifumo ya kiuchumi, kiutawala, kibiashara na asasi zote zinazounga mkono itikadi ya utandawazi huzingatia masilahi ya waliozianzisha ambao ni watu wa mataifa ya Kimagharibi.

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni na maishani. Mwandishi anaonesha kuwa elimu ni muhimu duniani kote kwani hupanua na kumfanya awe na akili iliyopevuka. Mwalimu wa kina Afida kule Motoni alikuwa amepevuka kiakili, ndiyo maana alikuwa na uwezo wa kuwaonya dhidi ya utashi wa vitu. Mtunzi anaendeleza dhana hii ya elimu ya akademia kwa kuonesha umuhimu wa fasihi, kwani Afida anamkumbuka mwalimu wao wa fasihi kule Motoni kuonesha mafunzo ya mwalimu wake yaliyomwathiri sana hata akiwa Motoni. Afida anasoma Peponi na kuweza kuhitimu na kutuzwa zawadi kwa kuwa mwanafunzi wa kwanza wa Motoni kufaulu vizuri na kupewa fursa ya kutoa hotuba ya shukrani. Hii inaonesha kuwa Mwafrika anaweza kusoma ughaibuni na kufaulu vizuri kuliko wanafunzi wa huko. S. A. Mohamed anadhihirisha kuwa itikadi ya utandawazi haijali rangi ya mtu bali uwezo wake wa kiakili ndiyo humwezesha kufasiri dhana za kiakademia (uk. 96). Kwa mfano, Profesa Marjan alikuwa amesoma hadi akafuzu kuwa profesa na kupata kazi ya kusomesha Chuo Kikuu cha Peponi licha ya kuwa asili yake ni “Motoni” (uk157).

Aidha, Mohamed anazungumzia dhana ya ugonjwa hasa unaoathiri dunia nzima. Sada, dada yake Afida aliaga dunia kutokana na ugonjwa usiopona wa UKIMWI. Aidha, Shuhuda rafikiye Afida alishikwa na ugonjwa usiokuwa na tiba hatimaye anaaga dunia (uk. 161)**.** Mtunzi anaonesha jinsi ugonjwa wa UKIMWI ulivyoathiri dunia nzima kutokana na madhara ya utandawazi na jinsi ulivyosambaa kote duniani ikiwamo Afrika na Ulaya. Pia, anaonesha namna watu wanaoishi maisha ya ovyo, mfano ukahaba kama kina Shuhuda, wako katika hatari ya kuangamia kutokana na UKIMWI. Mwandishi anaamini kuwa kuwapo kwa magonjwa hayo ni mojawapo ya athari za utandawazi.

Utamaduni ni mtindo wa maisha unaotambulisha kundi fulani la watu kwa lugha, tabia, na mila zao; na pia mfumo mzima wa maisha ya jamii hiyo. Utamaduni unahusisha tabia, lugha ya mwili, mahusiano na salamu. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, mwandishi anaonesha namna utamaduni wa jamii ya Motoni na Peponi ulivyokuwa. Kule Motoni, Shaabani haruhusiwi kumkumbatia Afida mbele ya wazee au jamaa zake licha ya kuwa mpenzi wa pekee wa Afida anayejulikana na jamaa yake. “Shaabani alimsogelea Afida, alitamani kumvamia na kumkumbatia lakini madhehebu ya utamaduni hayakumruhusu….” (uk 14). Jamii ya kina Afida na jumuiya yao iliruhusu wasichana kuvaa buibui ambayo haioneshi mkatiko wa mwili na kuwahimiza kufunga khanga kutokea kichwani hadi miguuni na kujifunika mtandio.

Mtunzi anaonesha kuwa misingi ya kitamaduni imesambaratika. Afida baada ya kukaa Peponi kwa muda alisahau ahadi zake kwa jamaa zake na akamsahau mchumba wake, Shaabani na akaanza kunywa vileo. Afida akaolewa na Nesboch, akapata mtoto nje ya ndoa, baadaye anatalikiwa na akapata mtoto mwingine. Hakulipiwa mahari na arusi ilihudhuriwa na watu wachache tu wa familia yao. Mambo haya yanadhihirisha kwamba aliasi utamaduni wa Kiafrika (Motoni) na kufurahia maisha ya Ulaya (Peponi). Mtunzi anaonesha kuwa utamaduni hauna mashiko tena yaani watu hutenda vile wanavyotaka mradi malengo yao ya kibinafsi yanatimizwa ambayo ni mawazo ya kiulimwengu wakati huu.

Mohamed ameongozwa na itikadi ya utandawazi kusawiri dhana ya ndoa. Ametuonesha kuwa ndoa inaweza kuwa baina ya Wazungu na Waafrika pia. Mwafrika yeyote anaweza kuolewa na Mzungu kwani siku hizi dunia imekuwa kama kijiji. Watu wanaweza kukutana kwa urahisi kwa sababu teknolojia inarahisisha mawasiliano kupitia simu na kompyuta na pia kurahisisha usafiri kupitia ndege. Bi Marneti ambaye ni Mwafrika ameolewa na Bw. Bawa ambaye ni Mzungu na Afida ambaye ni Mwafrika ameolewa na Neshboch ambaye ni Mjerumani. Sio lazima Mwafrika amuoe Mwafrika ndiyo maana Mohamed alituangazia kuhusu Yakrobich mwenye asili ya Kiafrika akikataliwa na Afida (Mwafrika mwenzake) na badala yake anaolewa na Mzungu Neshboch.

Mohamed kwa kuzingatia dhana ya utandawazi, anatuangazia jinsi ndoa zote zinavyofanana, iwe nchi ya Afrika au ya ng’ambo. Misukosuko ya ndoa iko sawia haijalishi mahala mulipo. Ndoa za Kiafrika na ndoa za nchi za ng’ambo hukumbwa na matatizo kama vita, ugomvi, fitina na talaka. Mohamed anatumia wahusika katika ndoa kuangazia mambo haya. Mfano, ndoa ya Afida na Neshboch inaishia katika talaka. Ndoa hii pia ilikumbwa na fitina kutoka kwa Bi. Marneti na Bi. She-iza. Mohamed kwa upande mwingine anataka kutuonesha jinsi kizazi kipya cha siku hizi kisivyothamini kanuni za ndoa. Anaelekeza kuwa ndoa yapaswa kulindwa kwani ni asasi muhimu. Mwanamke anapaswa kupata mtoto ndani ya ndoa sio nje ya ndoa kama alivyofanya Afida na Neshboch. Aidha, kulingana na sheria za ndoa, mke anapaswa kutumia jina la mume wake. Hii inaonesha kwamba ndoa na familia ulimwenguni kote ni asasi ya kiitikadi ya kumnyamazisha mwanamke, na kumfanya mnyenyekevu kuambatana na itikadi tawala (Althusser, 1981).

Inavyodhihirika ni kuwa, mtunzi anaamini katika mawazo ya kiulimwengu kuhusu ndoa kuwa ni baina ya watu wawili na yule wa tatu anapojitokeza basi matatizo mengi huzuka. Hili huwezekana kwa sababu katika ndoa nyingi katika nchi za Ulaya watu hukaa wawili, yaani mume na mke bila kuingiliwa na watu wengine

kifamilia. Hata hivyo, hapa Afrika mara nyingi watu wa familia hukaa pamoja na jamaa zao wa familia kama shangazi, shemeji binamu na wengineo. Mtunzi anaonekana kuamini katika ndoa ambayo watu hawakai pamoja na jamaa zao. Haya ni mawazo ya kiutandawazi au kiulimwengu ambapo watu wengi duniani wanaamini kuwa ili ndoa idumu wawili waliooana wanapaswa kuishi hivyo, yaani familia ya baba, mama na watoto kama wapo.

Mtunzi pia anaonesha ndoa kati ya Afida na Neshboch ambapo Afida alishawishiwa kukubali kuolewa na mzee Neshboch licha ya kumzidi kiumri. Alikuwa kama rika ya baba yake mzazi Afida, miaka sitini na miwili (uk. 138). Afida alikuwa na mpenzi mwingine Yakrobich ambaye walikuwa wa rika moja lakini kutokana na ushawishi wa Bi Marnet, anakubali kuolewa na Nesboch. Ndoa hii kwa Afida ilikuwa ni kivukio cha kupata uraia wa kuishi Peponi. Hii inaonesha namna ambavyo mali na utajiri huweza kumwathiri mtu yeyote katika maamuzi yake. Hali hii inawakilisha imani ya mtunzi kuwa, wasichana wengi wa kilimwengu siku hizi wana tamaa ya mali na utajiri, na kwa hivyo, ndoa zenye msingi imara wa mapenzi na ukweli ni muhali kupatikana hasa barani Afrika.

Aidha, katika suala zima la ndoa mtunzi hajaonesha kuhusu malipo ya mahari ama kuhusishwa kwa wazazi kabla ya ndoa kufungwa. Haya yote yanadhihirisha kuwa msimamo wa Mohamed kuhusu ndoa umeongozwa na itikadi yake ya utandawazi. Anaonesha kwamba watu wanaingiliana na kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kuoana kutoka mataifa tofauti na asili tofauti. Kwa hivyo, dhana ya wazazi kuhusika katika masuala yahusuyo ndoa na mahari yanatupiliwa mbali. Aidha, wanapoachana wanaenda kortini na kupata uamuzi huko badala ya kupata ushauri wa wazazi. Haya yote yanaonesha kuwa Mohamed anaongozwa na itikadi ya utandawazi.

Kuhusu dini, mwandishi anasema kuwa, Afida na familia yake walikuwa waumini wa dini ya Kiislamu na alilazimika kuvaa baibui. Babake hakuchelea kumhimiza Afida kumshukuru Mungu na kupenda dini yake, na kila mara katika mazungumzo yake na Afida, hakusita kumhimiza jinsi Mungu alivyotenda mema (uk. 118). Vilevile, Darwesh (babake Afida) anaendeleza vyema jambo hili la dini, kwani tunafahamishwa kuwa alikuwa kiongozi wa kidini. Hii ni kutokana na imani katika utandawazi ambapo katika ulimwengu mzima sasa, masuala ya dini na viongozi wa kidini hayachukuliwi kuwa ndiyo ukweli, kwani misimamo ya kidini inaonekana kusambaratika.

Mohamed pia anatuonesha kuwa dini haiwezi ikamkomboa mtu katika ulimwengu wa kisasa, bali mtu binafsi ndiye anayepaswa kujikomboa na nafsi yake. Hii ina maana kuwa, mtu binafsi ndiye huweza kuamua afanye lipi, aache lipi, wala sio misingi ya kidini ambayo haina mashiko katika ulimwengu wa kisasa. Hali hii inamfanya Afida kufanya uamuzi wa kupata mtoto nje ya ndoa, kuolewa na Nesboch ambaye ni Mkristo, kunywa vileo na kufanya mambo bila ya kuzingatia misingi yoyote ya kidini. Haya pia yanadhihirisha kuwa mtunzi anaridhia itikadi ya utandawazi ambapo mtu binafsi hufanya maamuzi kwa kuzingatia utashi binafsi na uhuru wa fikra zake.

Sheria za Peponi zinakubali serikali kumpa pesa mwanamke ambaye amelemewa kumlea mtoto wake ili aweze kujikimu kimaisha na mwanawe. Hili linadhihirika pale serikali ya Peponi ikimfadhili Afida pesa za kumtunza mtoto kwa kuwa hakuwa na kazi rasmi ya kufanya ili kupata kipato. Sheria ya Peponi, kama Afida alivyotambua baadaye, ilikuwa na upendeleo. Hii inaonesha kuwa katika mataifa yote asasi za utawala, kama vile sheria na mahakama, hutumiwa na wenye uwezo kuendeleza na kulinda maslahi yao. Afida hakupata haki katika mahakama. Sheria inatumiwa kumdhulumu, kwani hata Neshboch hakushtakiwa wala kuhukumiwa kwa kumpiga na kumuumiza Afida nusura afe. Sheria na mahakama ni vyombo tu vya kuendeleza itikadi tawala kwa kuwanyamazisha wanaodai haki zao.

Mtunzi pia amezungumzia mfumo wa kuumeni. Mwanamke amechorwa kwa vigezo viwili vikuu; vya uzuri na ubaya. Tukiegemea katika kitengo cha wanawake kuwa wazuri, hili linadhihirishwa na shangazi yake Afida, Bi Sinangoa ambaye hakuchelea kumsaidia Afida alipokuwa anasoma, kwa sababu wazazi wake Afida mara nyingi hawakuwa na hela za kutosha za kuikimu familia. Bi Sinangoa alikuwa akiingilia na kumsaidia Afida**.** Aidha, mke wa Profesa Marjan (Maryam) alikuwa kama mamake wa kupanga. Afida alimwendea na kumwambia kuwa alikuwa ni mjazito na ilimpasa aache masomo ya Chuo Kikuu ili amlee mtoto wake. Maryam alikuwa tayari kumlelea mtoto ili aendelee na masomo yake (uk. 158). Aidha, Afida alikuwa na msimamo thabiti hakuingia katika mtego wa Sapataro, Bw. Bawa au wa Yakrobich, ambao walijaribu kwa lolote lile kumnasa katika mtego wao wa mapenzi ya uongo (uk. 123). Hili linadhihirisha mawazo ya mtunzi kuwa kuna tofauti kubwa baina ya mapenzi na urafiki. Afida alikuwa na msimamo wake kuwa urafiki haumaanishi kushiriki ngono. Mawazo haya yanaafikiana na mtazamo wa kiutandawazi ambapo watu wana uhusiano wa kirafiki na jinsia tofauti bila kushiriki ngono. Aidha, mtunzi anadhihirisha kuwa Afida na mamaye Bi Mwamda ni watu wenye bidii katika kazi zao.

Mtunzi pia amezungumzia kudunishwa kwa mwanamke katika riwaya hii. Katika nchi ya "Peponi" wanawake wa asili ya Kiafrika wanadunishwa sana kwa kuwa wengi wanachorwa kama vyombo vya kumaliza ashiki ya wanaume. Wanawake wenyewe wanashikilia jambo hili na kulitenda bila kujali. Saparata alikuwa na matamanio ya kimwili na Afida (uk. 85). Hii inaashiria kuwa wanawake walichukuliwa kama chombo cha kumaliza ashiki za wanaume na mtazamo huo unaathiri namna wanavyoiona jinsia ya kike, yaani kama kitu cha

"kuliwa" tu na kuachwa, wala sio binadamu kamili**.** Hali hii inasababishwa na mfumo wa kuumeni ambapo wanaume huonesha kuwa wao ndio viumbe bora zaidi duniani ilhali jinsia ya kike haina thamani yoyote. Neshboch anamfunza mwanawe wa kiume Dinda kuwa, wanawake hawana thamani yoyote na kuwa wanaume ndio walio na mamlaka na maana zaidi duniani (uk. 163). Hii inaonesha kuwa mfumo wa kuumeni ni kigeu au asasi ya kiitikadi kinachotumiwa kuhalalisha udhalilishaji wa jinsia.

Mohamed pia ameonesha ubaguzi wa rangi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Hiki ni kitendo cha kuthamini au kutenga binadamu kwa misingi ya rangi za ngozi. Hii ni dhana ya kumbagua mtu kulingana na rangi ya ngozi yake. Binadamu huwa na rangi ya ngozi ya aina mbili; mweusi au mweupe. Waafrika huwa weusi ilhali Wazungu huwa weupe. Ubaguzi wa rangi ulikuwa maarufu sana katika nchi kama Afrika Kusini na Marekani ambapo Waafrika walikandamizwa kutokana na rangi yao. Wakati wa Ukoloni barani Afrika, rangi ilitumika kama msingi wa utoaji huduma muhimu na haki nyingine za kibinadamu. Rangi nyeusi ilipewa hadhi ya chini zaidi. Aidha, Visiwani Zanzibar, rangi ilitumiwa kumuweka mtu katika tabaka fulani, kwa mfano, Rehema katika *Nyota ya Rehema*, Fuadi alimkataa kutokana na weusi wake. Siku hizi, takribani nchi zote, sheria za kupinga ubaguzi wa rangi zimewekwa, lakini katika nchi nyingi, bado kuna wabaguzi wachache ambao wanavunja sheria kwa kuendelea kubagua kwani ni asasi mojawapo cha kiitikadi (Gramsci, 1981). Afida alibaguliwa na Wapeponi kwa sababu ya rangi yake. Alikuwa mweusi, ilhali wao Wapeponi ni waeupe. Afida alibaguliwa kila mahali sio shuleni bali pia katika basi na hata katika ndoa yake (uk. 90). Dinda ambaye alikuwa mchanganyiko wa asili ya Kiafrika na Kizungu, alibaguliwa sawia na Waafrika wenzake. Jambo hili ni dhihirisho kuwa ubaguzi wa rangi ni kigeu tu cha kuiendeleza itikadi tawala.

## IV. HITIMISHO

Kwa ujumla, makala hii imeonesha jinsi itikadi ya utandawazi inavyojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kama iivyodhihirishwa katika vipengele vya mfumo wa kiuchumi, kielimu, kindoa, kidini, asasi za utawala, kimaadili na mfumo wa kuumeni. Pia, imeonesha kuwa, mtunzi anapendekeza mapinduzi kufanyika ili kusuluhisha matatizo yao kwani kutorokea mataifa ya Ulaya hakubadilishi hali. Kwa hakika, Mohamed anaupinga utandawazi na kuonesha namna unavyoathiri mataifa machanga ya Kiafrika. Mtunzi ameonesha kuwa matumaini ya ukombozi yapo lakini si kupitia utandawazi. Waafrika wajinasue kutokana na itikadi hii ya utandawazi na wafanye mambo yao wenyewe. Kwa hiyo, itikadi inayotawala katika riwaya zote mbili ni utandawazi. Hata hivyo, mwandishi anadokeza itikadi ya mapinduzi ili kuukabili utandawazi katika nchi zinazoendelea.

## MAREJELEO

[1]. Althusser, L (1981). Ideology and Ideological State Apparatuses katika *Lenin and Other Essays.*
[2]. Mtafsiri. B. Brewster. London: New left Books.
[3]. Ardono, T. (1950). *The Authoritarian Personality*. New York: Haper.
[4]. Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert.* Dar es Salaam: TATAKI.
[5]. Derrida, J. (1976). *Of Grammatology and Writing and Difference*. Mtafsiri. G. C. Spivak. Baltmore: John Hopkins.
[6]. Gramsci, A. (1971). *Selections from Prison Note Books*. New York: International Publishers.
[7]. Gramsci, A. (1985). Selections from Cultural Writings, katika D. Forgas and G. Nowel- Smith (Wafs.). London: Lawrence and Wishart. kur. 389-390.
[8]. Jesse, M. (2017).Itikadi Katika Riwaya za S.A Mohamed.Tasnifu ambayo Haijachapishwa:Chuo Kikuu cha Kenyatta
[9]. Lowenstein, K. (1953). "The Role of Ideologies in Political Change." International Social Science Bulletin, 5 (1): 51-74.
[10]. Marx, K. na F. Engels. (1973). *On Literature and Art*. New York: International General
[11]. Marx, K na F. Engels.(1977). *The German Ideology.* London: Lawrence and Wishar.
[12]. Mbatiah, M. (1997). Commitment in the Swahili Novel: An Appraisal of the Works of Said Ahmed Mohammed katika D. P. B. Massamba and Mulokozi, M. M. (Wah.) *Kiswahili*.
[13]. Dar-es-Salaam: TUKI. 6:75-80
[14]. Mbatiah, M. (1999). The Origin and Development of the Swahili Theses Novel in Tanzania Tasnifu ambayo Haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
[15]. Mohamed, S. A. (1978). *Asali Chungu.* Nairobi: Shungwaya.
[16]. Mohamed, S. A. (1980). *Utengano.* Nairobi: Longhorn.
[17]. Mohamed S. A. (1986). *Kiza katika Nuru.* Nairobi: Oxford University Press.
[18]. Mohamed S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi.* Nairobi: E.A E. P.
[19]. Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
[20]. Mohamed S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

[21]. Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: U. O. N. Press.
[22]. Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: J. K.F.
[23]. Rossiland, F. (1990). *Marxism and Ideology.* Oxford: Clarendon Press.

Jesseemurithii,.'' Itikadi katika Riwaya za Dunia Yao (2006) na Mhanga Nafsi Yangu (2013) za S. A. Mohamed." IOSR Journal Of Humanities And Social Science (IOSR-JHSS). vol. 23 no. 09, 2018, pp. 39-46